
UFUNUO 3

COMIC BIBLE
SOCIETY

Published by the Comic Bible Society, LLC
Copyright © 2023

Kingstone Comics maintains copyright to this comic book as provided by United States copyright law.

Print and digital copies of this version may be freely distributed without penalty under a Creative Commons license.


"HATA WATAKAPOUMALIZA USHUHUDA WAO, YULE MNYAMA [1] ATOKAYE KATIKA KUZIMU ATAFANYA VITA NAO..."
"NAYE ATAWASHINDA NA KUWAUA, NA MAITI ZAO ZITAKUWA KATIKA NJIA YA MJI ULE MKUU, AMBAPO BWANA WAO ALISULUBIWA."
NA WATU KUTOKA KOTE ULIMWENGUNI WATATAZAMA MAITI ZILIZOKUWA NJIANI KWA SIKU TATU NA NUSU."
HATIMAYE, WATESI HAWA WAWILI WAMEONDOKA.
[1] MARA YA KWANZA KATI YA 36 MOINGA KRISTO ATAJWA. ANATOKA SHIMO LA JEHANAMU NA NGUVU ZAKE NI ZA KISHETANI.


TUKIO ZIMA LINAREKODIWA KWENYE HABARI ILI ULIMWENGU MZIMA UONE.
WANASTAHILI! NASHKURU WAMETUONDOKEA NA MAZUNGUMZO YAO YA AKILI FUPI.
NANI ANAYEJALI KUHUSU KIUMBE HUYU ANAYESEMEKANA KUWA WA KUINGU - TUMECHOKA NA NJIA ZAKE ZISIZO VUMILIVU!
SASA TUSHEREHEKEE!
"NAO WAKAAO JUU YA NCHI WASHANGILIANA KUPEANA ZAWADI WAO KWA WAO..."
"...KWA KUWA WALIKUWA WAMETESWA NA MANABII HAO WAWILI."
UFUNUO 11:7-10


"LAKINI ROHO YA UHAI ITOKAYO KWA MUNGU IKAWAINGIA."
"NA WAKASIMAMA KWA MIGUU YAO."
NINI --?
HAIWEZEKANI....
WALISEMA KUWA MUNGU ATA....
"NA WAKASIKIA SAUTI KUU KUTOKA MBINGUNI IKIWAAMBIA..."
PANDENI HUKU!
...FUFUA WAFU, WATAKATIFU NA WASIO WATAKATIFU...
"NA WAKAPANDA MBINGUNI KATIKA WINGU, ADUI ZAO WAKIWATAZAMA."
HAIWEZEKANI...
NIMEKUWA NIKIWAZA WALICHOKISEMA - LABDA NI KWELI?!
LAZIMA KUNA NJIA YA KUELEZA HAYA.
UFUNUO 11:11-12







UFUNUO 11:13-14


"MALAIKA WA SABA AKAPIGA BARAGUMU, PAKAWA NA SAUTI KUU MBINGUNI, ZIKISEMA, 'UFALME WA DUNIA UMEKWISHA KUWA UFALME WA BWANA WETU NA WA KRISTO WAKE, NAYE ATAMILIKI HATA MILELE NA MILELE.'"
"KISHA HEKALU LA MUNGU LILILOKO MBINGUNI LIKAFUNGULIWA, NA SANDUKU LA AGANO LAKE LIKAONEKANA NDANI YA HEKALU LAKE."
"KUKAWA NA UMEME, NA SAUTI, NA RADI, NA TETEMEKO LA NCHI, NA MVUA YA MAWE NYINGI SANA."


TUNAKUSHUKURU WEWE BWANA MUNGU MWENYEZI, ULIYEKO NA ULIYEKUWAKO, KWA SABABU UMEUTWAA UWEZA WAKO ULIO MKUU, NA UKAANZA KUMILIKI.
MATAIFA YALIKASIRIKA...
...HASIRA YAKO NAYO IMEKUJA.
WAKATI UMEFIKA WA KUWAHUKUMU WALIOKUFA...
...NA KUWAPA THAWABU WATUMWA WAKO MANABII....
...NA WATAKATIFU WAKO NA WALICHAO JINA LAKO, WADOGO KWA WAKUBWA...
...NA KUWAHARIBU HAO WANAOIHARIBU NCHI.
UFUNUO 11:15-17


"NA ISHARA KUU ILIONEKANA MBINGUNI: MWANAMKE ALIYEVIKWA JUA, NA MWEZI ULIKUWA CHINI YA MIGUU YAKE, NA JUU YA KICHWA CHAKE TAJI YA NYOTA KUMI NA MBILI." [1]
"NAYE ALIKUWA ANA MIMBA, AKILIA, HALI ANA UCHUNGU NA KUUMWA KATIKA KUZAA."
[1] HII NI ISHARA YA KWANZA KATI YA SABA KATIKA NUSU YA KWANZA YA UFUNUO.
MWANAMKE NI TASWIRA YA ISRAELI KARIKA MAANDIKO.
JUA NI USRAELI INAVYOTUKUZWA NA KUINULIWA.
NYOTA KUMI NA MBILI ZINAASHIRIA KABILA KUMI NA MBILI ZA ISRAELI.


UFUNUO 12:1-2




[1] KATIKA UASI WA KWANZA WA IBILISI, THELUTHI YA MALAIKA WALIJIUNGA NAYE (ISAYA 14:12, EZEKIELI 28:1).

[2] KUTOFANIKIWA KATIKA KUZUIA KUZALIWA WAKIBIKRA WA KRISTO, IBILISI ALIJARIBU KUSABABISHA KUUWAWA KWAKE KATIKA MAUAJI YA WATOTO WA KIUME NA HERODE HUKO BETHLEHEMU.

[3] YESU NI WA KIZAZI CHA UYAHUDI NA YA KIMASSIAH NA NI MFALME MWENYE NGUVU JUU YA MATAIFA YOTE ULIMWENGUNI.

[4] KUPAA KWA KRISTO (MATENDO 1:9, 2:33).

[5] MUNGU AMLINDA MWANAMKE (ISRAELI) KWA KUMLINDA NYIKANI, YAWEZEKANI SEHEMU ZA MOABU, AMONI NA EDOM KWANI ZINAACHWA KATIKA MASHAMBULIZI YA MPINGA KRISTO DHIDI YA NCHI TAKATIFU (DANIELI 11:41).




[1] IBILISI NA MALAIKA WAKE WALITUPWA NJE KUTOKA MBINGUNI KWA UASI WAO WA KWANZA ILA BADO WANA UWEZO WA KUINGIA (AYUB 1:6, 2:1). SASA WAMEZUILIWA MILELE KUINGIA MBINGUNI.

[2] MABAWA YA TAI NI UWEPO WA MUNGU UNAOLINDA.

[3] INGAWA JESHI KUU LAJA DHIDI YA ISRAELI KAMA MAFURIKO (YEREMIA 46:8, 47:2) ITAMEZWA - KUNA UWEZEKANO MKUBWA KATIKA MOJA YA MITETEMEKO YA ARDHI ITAKAYOFANYIKA WAKATI HUU.



"...LAKINI ALISHINDWA, NA WAKAPOTEZA NAFASI YAO MBINGUNI."[1]
"YULE JOKA MKUBWA, AUDANGANYAYE ULIMWENGU WOTE, AKATUPWA KWENYE NCHI - NA MALAIKA ZAKE WAKATUPWA PAMOJA NAYE."
"MWANAMKE YULE AKAPEWA MABAWA MAWILI YA TAI YULE MKUBWA [2] ILI ARUKE, AENDE ZAKE NYIKANI, HAPO ATAKAPOANGALIWA KWA WAKATI WA MIAKA MITATU NA NUSU, MBALI NA NYOKA HUYO.
"JOKA AKAMKASIRIKIA YULE MWANAMKE, AKAENDA ZAKE AFANYE VITA[3] JUU YA WAZAO WAKE - WAZISHIKAO AMRI ZA MUNGU, NA KUWA NA USHUHUDA WA YESU."
UFUNUO 12:7


"NAYE AKASIMAMA JUU YA MCHANGA WA BAHARI [1] KISHA NIKAONA MNYAMA AKITOKA KATIKA BAHARI." [2]
"KIMOJA CHA VICHWA VYAKE MNYAMA YULE KANA KWAMBA KIMETIWA JERAHA LA MAUTI, NA PIGO LAKE LA MAUTI LIKAPONA." [3]
"ALIKUFURU MUNGU NA JINA LAKE, MAKAO YAKE NA WOTE WANAOISHI MBINGUNI."
[1] MICHANGA YA BAHARI YAONYESHA KUWA MPINGA KRISTO ACHUKUA MAHALA PAKE KATI YA MATAIFA YOTE ULIMWENGUNI.
[2] BAHARI INAWAKILISHA SHIMO WATOKAKO MAPEPO. IBILISI ANAMUITA PEPO MWENYE NGUVU ALIYE NDANI YA MNYAMA NA AMUONGOZAYE.
[3] HII NI KAMA KIFO NA KUFUFUKA KWA UONGO KULIKOIGWA NA MPINGA KRISTO KAMA NJIA YAKE YA ULAGHAI MKUU.
[4] WAKATI HUU ATAKUBALIWA KUWACHINJA NA KUWAUA WALE WANAOMFUATA NA KUMPENDA MUNGU.


"ALIPEWA UWEZO WA KUWASHINDA WATAKATIFU NA ALIPEWA MAMLAKA JUU YA MATAIFA YOTE." [4]
WAKAAZI WOTE WA NCHI WATAMUABUDU MNYAMA - WOTE AMBAO MAJINA YAO HAYAJAANDIKWA KWENYE KITABU CHA UHAI CHA MWANA-KONDOO.
UFUNUO 13:1-10




[1] MPINGA KRISTO CHA MSINGI NI KIONGOZI WA KIJESHI NA KISIASA, LAKINI NABII WA UONGO NI KIONGOZI WA KIDINI NA PIA ATATUMIA NGUVU ZA KISHETANI.

[2] ISHARA KUU - MANENO YALE YALE YANAYOTUMIKA KUELEZA MIUJIZA YA YESU. NABII MUONGO ATAFANYA ISHARA ZINAZOIGA ZILE ZA KRISTO.

[3] AINA YA MFANO WA MPINGA KRISTO WAWEKWA NDANI YA HEKALU YA YERUSAELMU - CHUKIZO LA UHARIBIFU (MATHAYO 24:15-16).

[4] NAMBARI HUONYESHA USAHIHI WA MUNGU NA ZAWAKILISHA MAWAZO. SABA NI NAMBARI YA UKAMILIFU NA SITA NI NAMBARI YA BINADAMU - KUPUNGIKIWA NA UKAMILIFU. MPINGA KRISTO HATIMAYE AKIFUNULIWA KUTAKUWA NA NJIA YA KUMTAMBUA NA NAMBARI YAKE.


"AKAPEWA UWEZO WA KUTIA PUMZI KATIKA ILE SANAMU YA MNYAMA WA KWANZA, ILI INENE, NA KUWAFANYA HAO WOTE WASIOISUJUDU SANAMU YA MNYAMA WAUAWE." [3]
"ALIWALAZIMU WATU WOTE WATIWE CHAPA KATIKA KATIKA VIPAJI VYA NYUSO ZAO AU MKONO WAO WA KUUME ILI KWAMBA MTU YEYOTE ASIWEZE KUNUNUA WALA KUUZA, ISIPOKUWA ANAYE CHAPA ILE, YAANI JINA LA MNYAMA YULE AU HESABU YA JINA LAKE."
"NAMBARI YA MNYAMA NI NAMBARI YA KIBINADAMU - NI 666." [4]
UFUNUO 13:11-18


KISHA NIKAONA, NA TAZAMA, HUYO MWANA-KONDOO AMESIMAMA JUU YA MLIMA SAYUNI PAMOJA NA WATU 144,000 WENYE JINA LAKE NA JINA LA BABA YAKE LIMEANDIKWA KATIKA VIPAJI VYA NYUSO ZAO." [1]
[1] IBILISI ATUPA NAMBARI - LAKINI MUNGU ATUPA JINA. WAFUASI WA MPINGA KRISTO WANA NAMBARI YAKE ILIYOANDIKWA KATIKA VIPAJI VYA NYUSO ZAO, LAKINI WAFUSAI WA KRISTO WANA JINA LAKE KWENYE VIPAJI VYA NYUSO ZAO.
[2] WIMBO WA UKOMBOZI WAIMBWA, KUFURAHIA KATIKA KAZI YOTE YA UKOMBOZI WA MUNGU.
[3] WANABAKI WASAFI KATI YA UGUMU MKUU ULIMWENGUNI.
[4] WANAZUNGUMZA UKWELI WA MUNGU KWA UKAMILIFU NA USAHIHI.


"NAMI NIKASIKIA SAUTI KUTOKA MBINGUNI KAMA SAUTI YA MAJI MENGI, NA KAMA SAUTI YA RADI KUU."
"NA HIYO SAUTI NILIYOISIKIA ILIKUWA KAMA SAUTI YA WAPIGA VINUBI, WAKIVIPIGA VINUBI VYAO, NA KUIMBA WIMBO MPYA MBELE YA KILE KITI CHA ENZI, NA MBELE YA WALE WENYE UHAI WANNE, NA WALE WAZEE." [2]
"WALA HAPANA MTU ALIYEWEZA KUJIFUNZA WIMBO ULE, ILA WALE 144,000."
HAWA NDIO WASIOTIWA UNAJISI PAMOJA NA WANAWAKE, KWA MAANA NI BIKIRA NA NDIO WAMFUATAO MWANA-KONDOO KILA AENDAKO." [3]
"HAWA WAMENUNULIWA KATIKA WANADAMU, MALIMBUKO KWA MUNGU NA KWA MWANA-KONDOO. NA KATIKA VINYWA VYAO HAUKUONEKANA UONGO. MAANA HAWANA MAWAA." [4]
UFUNUO 14:1-5




[1] MALAIKA HUYU AWAAMBIA BINADAMU WATAKAYEMUOGOPA - SIO IBILISI, SIO MAPEPO, SIO MAJANGA BALI KUMUOGOPA KUMPA MUNGU NA KUMPA HESHIMA.

[2] UKOSEFU WA JIBU KUTOA MALAIKA WA KWANZA KULIMSABABISHA MUNGU KUTUMA MALAIKA WA PILI MKUU NA MWENYE UJUMBE WA KUTUBU.

[3] MJI WA KIASILI WA BABELI ULIKUWA KITOVU CHA IBADA YA SANAMU.

SASA MUNGU AHUKUMU UFALME MZIMA WA KISIASA, KIUCHUMI NA KIDINI WA MPINGA KRISTO KOTE ULIMWENGUNI AMBAO UMEKUWA UZUSHI WA UASI DHIDI YA MUNGU.

[4] MALAIKA WA TATU ATAMKA HATIMA NA UHAKIKA WA HUKUMU YA MUNGU.

HASIRA YA MUNGU SIO MLIPUKO WA GHAFLA ILA NI JIBU DHABITI NA LISILO NA HURUMA LA MUNGU MWENYE HAKI KWA WALE WANAOKATAA KUJIBU IMANI NDANI YA KRISTO ANAYOITOA KWA NEEMA.




UFUNUO 14:6-13


TIA MUNDU WAKO UKAVUNE, KWA KUWA SAA YA KUVUNA IMEKUJA NA MAVUNO YA NCHI YAMEKOMAA!
[1] VITA VYA HAR-MAGEDONI NI VYA DAMU NYINGI MPAKA DAMU INATAPAKAA FUTI NNE JUU (HATAMU YA FARASI) NA KUNA MITARO YA DAMU UNDANI HUO HUO.


TIA MUNDU WAKO MKALI UKACHUME VICHALA VYA MZABIBU WA NCHI, MAANA ZABIBU ZAKE ZIMEIVA SANA.
"MALAIKA YULE AKAUTUPA MUNDU WAKE HATA NCHI, AKAUCHUMA MZABIBU WA NCHI, AKAZITUPA ZABIBU KATIKA SHINIKIZO HILO KUBWA LA GHADHABU YA MUNGU."
"SHINIKIZO LILE LIKAKANYAGWA NJE YA MJI, DAMU IKATOKA KATIKA SHINIKIZO MPAKA KWENYE HATAMU ZA FARASI, KAMA MWENDO WA MAILI "[1]


"KISHA NIKAONA ISHARA NYINGINE KATIKA MBINGU, ILIYO KUBWA, NA YA AJABU - MALAIKA SABA WENYE MAPIGO SABA YA MWISHO. MAANA KATIKA HAYO GHADHABU YA MUNGU IMETIMIA."
"TENA NIKAONA KITU KAMA MFANO WA BAHARI YA KIOO ILIYOCHANGAMANA NA MOTO, NA WALE WENYE KUSHINDA, WALIOMSHINDA YULE MNYAMA, NA SANAMU YAKE, NA KWA HESABU YA JINA LAKE, WALIKUWA WAMESIMAMA KANDO-KANDO YA HIYO BAHARI YA KIOO."
NI MAKUU, NA YA AJABU, MATENDO YAKO, EE BWANA MUNGU MWENYEZI!
NI ZA HAKI, NA ZA KWELI, NJIA ZAKO, EE MFALME WA MATAIFA!


MATAIFA YOTE WATAKUJA NA KUSUJUDU MBELE ZAKO KWA KUWA MATENDO YAKO YA HAKI YAMEKWISHA KUFUNULIWA.
NI NANI ASIYEKUCHA, EE BWANA, NA KULITUKUZA JINA LAKO? KWA KUWA WEWE PEKE YAKO U MTAKATIFU.
"WALIKUWA WAMESIMAMA KANDO-KANDO YA HIYO BAHARI YA KIOO, WENYE VINUBI WALIVYOPEWA NA MUNGU. WALIUIMBA WIMBO WA MUSA, MTUMWA WA MUNGU NA WIMBO WA MWANA-KONDOO."


"KUTOKA LILIPOKUWA HEKALU LA HEMA YA USHUHUDA NA PATAKATIFU ZAIDI WAKATOKEA WALE MALAIKA SABA NA VITASA VYA MWISHO VYA HUKUMU YA MUNGU." [1]
[1] TABIA YA MUNGU YA UTAKATIFU INALAZIMU AHUKUMU DHAMBI AMBAYO HAIKUTUBIWA.
VITASA NI SINIA ZISIZO NA KINA KIREFU KWA SABABU HUKUMU YA KIUNGU ITAMWAGWA PAPO HAPO KISHA KWA HARAKA.


HEKALU LIKAJAZWA MOSHI ULIOTOKA KWENYE UTUKUFU WA MUNGU NA UWEZA WAKE, HAPAKUWA ALIYEWEZA KUINGIA NDANI YA HEKALU, HATA YATIMIZWE MAPIGO SABA YA WALE MALAIKA SABA.
UFUNUO 15:5-8


"AKAENDA HUYO MALAIKA WA KWANZA, AKAKIMIMINA KITASA CHAKE JUU YA NCHI, PAKAWA NA MAJIPU MABAYA, MABOVU, JUU YA WALE WATU WENYE CHAPA YA HUYO MNYAMA, NA WALE WENYE KUISUJUDIA SANAMU YAKE." [1]
666


666
[1] WAFUASI WA MPINGA KRISTO WANATESWA NA MAJIPU YASIYOPONA, UCHUNGU NA YANAYOTOA MAJI. HILI NDIO NENO LA KIGIRIKI LINALOTUMIWA KUELEZA MAJIBU YALIYOWATESA WATU WA MISRI NA MAJIPU YALIYOMTESA AYUB.
UFUNUO 16:1-2




[1] BAADA YA VIFO VYA MABILIONI YA VIUMBE WA BAHARINI MAJI YANAGEUKA DAMU, MAZITO NA KUGANDA.

[2] ZAIDI YA KUTESEKA NA KIU KUTOKA NA UKAME ULIOKO ATAYARI ULIMWENGU, WANAOMSUJUDU MPINGA KRISTO HAWATAKUWA NA MAJI YA KUOSHA MAJIPU YAO.

[3] MALAIKA ASIFIA HUKUMU KALI YA MUNGU KULINGANA NA MATESO AMBAYO KIZAZI HILI KIKATILI AJABU KIMEFANYA WATAKATIFU NA MANABII KUYAPITIA.


"NAMI NIKAMSIKIA MALAIKA WA MAJI AKISEMA, 'WEWE U MWENYE HAKI, ULIYEKO NA ULIYEKUWAKO, MTAKATIFU, KWA KUWA UMEHUKUMU HIVI.'"
"KWA KUWA WALIMWAGA DAMU YA WATAKATIFU NA YA MANABII - NAWE UMEWAPA DAMU WAINYWE KAMA WANAVYOSTAHILI.'"[3]
"NIKAISIKIA HIYO MADHABAHU IKISEMA, "NAAM, BWANA MUNGU MWENYEZI, NI ZA KWELI, NA ZA HAKI, HUKUMU ZAKO."

UFUNUO 16:3-7


"MALAIKA WA NNE AKAKIMIMINA KITASA CHAKE JUU YA JUA, NALO LIKAPEWA KUWAUNGUZA WANADAMU KWA MOTO."
"WANADAMU WAKAUNGUZWA MAUNGUZO MAKUBWA, NAO WAKALITUKANA JINA LA MUNGU ALIYE NA MAMLAKA JUU YA MAPIGO HAYO; WALA HAWAKUTUBU WALA KUMPA UTUKUFU." [1]
NALILAANI JINA LA MUNGU KAMA ANAWEZA KUSABABISHA MATUKIO HAYA YA VITUKO.
LAKINI ULISEMA HAKUNA MUNGU - KUWA SOTE NI AJALI ZA MAZINGIRA NA MAZINGIRA YALIKUWEPO.
HII NI TOFAUTI - HII NI ISIYO YA KAWAIDA!
[1] AJABU, KATI YA JANGA BAYA JUU YA JANGA, WATU WANAKATAA KUTUBU UOVU WAO.


"MALAIKA WA TANO AKAKIMIMINA KITASA CHAKE JUU YA KITI CHA ENZI CHA YULE MNYAMA, UFALME WAKE UKATIWA GIZA. WATU WAKATAFUNA NDIMI ZAO KWA SABABU YA MAUMIVU." [1]
NIPE NAFUU!
UCHUNGU HUU HAUSTAHIMILIKI.
NAJIHISI KAMA AMBAYE NIKO JEHANAMU...
[1] KUMIMINWA KWA KITASA CHA TANO CHA HUKUMU KUNAKUJA KWA NJIA YA GIZA ZITO JUU YA UFALME MZIMA UNAOONGOZWA NA MPINGA KRISTO.
KAMA NI SABABU YA MWAKO WA JUA KUTOKA KITASA KILICHOPITA KUZIMA TEKNOLOJIA AU MACHINE AINA NYENGINE - NI HUKUMU MOJA KWA MOJA YA MUNGU KWA GIZA LA KIROHO LA BINADAMU NA MPINGA KRISTO.
UFUNUO 16:10-11


"MAIAIKA WA SITA AKAKIMIMINA KITASA CHAKE JUU YA MTO ULE MKUBWA FRATI, MAJI YAKE YAKAKAUKA, ILI NJIA ITENGENEZWE KWA WAFALME WATOKAO MASHARIKI." [1]
[1] MTIRIRIKO WAKE KAPUNGUA KWA SABABU YA UKAME NA HUKUMU, MTO MKUU WA FRATI UNAKAUKA KABISA - NA KUWAPA FURSA MUUNGANO NA JESHI LA KUTOKA MASHARIKI.
[2] MAJESHI YOTE ULIMWENGUNI YANAKUSANYIKA KATIKA NYIKA ZA MEGIDDO MAILI 60 KASKAZINI MWA YERUSALEMU.


"NIKAONA ROHO TATU ZA UCHAFU ZILIZOFANANA NA VYURA, ZIKITOKA KATIKA KINYWA CHA YULE JOKA, NA KATIKA KINYWA CHA YULE MNYAMA, NA KATIKA KINYWA CHA YULE NABII WA UONGO. HIZO NDIZO ROHO ZA MASHETANI, ZIFANYAZO ISHARA. ZASAFIRI NA KUWAENDEA WAFALME WA ULIMWENGU WOTE KUWAKUSANYA KWA VITA YA SIKU ILE KUU YA MUNGU MWENYEZI."
TAZAMA, NAJA KAMA MWIVI. HERI AKESHAYE, NA KUYATUNZA MAVAZI YAKE, ASIENDE UCHI HATA WATU WAKAIONE AIBU YAKE.
"KISHA WAKAWAKUSANYA WAFALME PAMOJA MAHALI PAITWAPO KWA KIEBRANIA, HAR-MAGEDONI. [2]
UFUNUO 16:12-16













SUPERBIBLE.TV